**HALMASHAURI YA MANISPAA YA LINDI**
**MTIHANI WA KISWAHILI DARASA LA IV, OKTOBA 2024**

## SEHEMU A: IMLA

1. Sikiliza sentensi zinazosomwa kisha ziandike kwa usahihi
   i. ______________________________________________________________
   ii. ______________________________________________________________
   iii. ______________________________________________________________
   iv. ______________________________________________________________
   **v.** ______________________________________________________________

## SEHEMU B: MATUMIZI YA LUGHA.

2. Chagua herufi ya jibu sahihi na kuandika katika kisanduku
   i. Katika neno alifagia, silabi **<u>li</u>** inaonesha wakati gani? A. ujao B.mtimilifu C. uliopita D. uliopita ( )

   ii. Vitu vinavyotengenezwa kutokana na miti huitwaje?
   A. thamani B. Samani C. Meza na vitanda D. Dhamani **( )**

   **iii.** Kinyume cha neno **"zima"** ni kipi kati ya vifuatavyo? A. Usizime B. Washa C. zimwa D. kuzimwa ( )

   iv. Kitendo cha **kuvuna asali** ni kipi kati ya hivi vifuatavyo? A. Kupakua B.Kuchota C.Kurina D.Kumimina ( )

   **v.** Wazazi wangu __________ nisome kwa bidii. A. walinionya B. walinihusia C. walinilazimisha D. waliniamrisha.( )

## SEHEMU C: METHALI, NAHAU NA VITENDAWILI

3. Kamilisha methali, nahau na tegua vitendawili vifuatavyo
   i. Nini maana ya kitendawili **"Para la mzungu lafuka moshi"** ________________________
   ii. Malizia methali hii, **Bandu bandu** ______________________________________________
   iii. Nini maana ya nahau **"Bwaga moyo"**? ____________________________________________
   iv. Nini maana ya nahau **"Onea kijicho"**? ____________________________________________
   **v.** Tegua kitendawili kifuatacho **"Pamparara, mlango wa chuma ukiufungua hauna huruma"**
   ______________________________________________________________

## SEHEMU D: UTUNGAJI

*4.* Tumia alama za uandishi zilizo katika mabano kukamilisha sentensi ulizopewa. Alama hizo ni, (**. , ! ? " "**)
   i. Utakuja lini kwetu________________________________
   **ii.** Nikifika sokoni nitanunua embe______ ndizi na parachichi.
   **iii.** Baba alisema,_____________ nitanunua gari___________
   **iv.** Looh__________________ kumbe Juma ni mtoto mtundu.
   v. Tulipofika sokoni tulinunua samaki___________________

## SEHEMU E: UFAHAMU

5. Soma habari ifuatayo kisha jibu maswali yatakayofuata:

Wakati ambao elimu kuhusu Dunia haijatambuliwa na wanadamu, watu hawakujua kuhusu Dunia yetu. Wapo walioamini kuwa Dunia ni tambarare kama meza, wengine waliamini ina umbo la mviringo na wengine walidhani Dunia haina kingo. Pia watu waliamini kuwa mtu anaweza kutembea hadi akafika mwisho wa Dunia na kuangukia kwenye shimo kubwa. Wengine waliamini kuwa kama ungepaa kwenda juu mwisho ungegusa mbingu. Baadaye, wataalamu wa mambo ya anga walithibitisha kuwa Dunia ina umbo la tufe . Pia wataalamu waliondoa utata wa kipi kati ya Dunia na jua kipi kinazunguka kingine, walibainisha kuwa Dunia ndiyo inayolizunguka jua kwa kuwa jua ni kubwa kuliko Dunia ila linaonekana na umbo dogo kwa kuwa lipo mbali sana na Dunia yetu.

### Maswali:

   i. Je ni kweli tunaweza kugusa mbingu? ____________________________________________
   ii. Wataalamu wa mambo ya anga wamethibitisha Dunia ina umbo la____________________
   iii. Kabla ya watu kuelimika waliamini Dunia ni ______________________________________
   iv. Watu waliamini kama mtu akitembea hadi mwisho wa Dunia nini kitatokea _____________
   v. Kati ya jua na Dunia kipi kinazunguka kingine? ______________________________________